

# THE SACRED NAME BROADCASTER

## Mtangazaji wa Jina Takatifu

3/2026

a publication of **Assemblies of Yahweh**

# THE SACRED NAME BROADCASTER

*An **Assemblies of Yahweh** publication.*
***Assemblies of Yahweh**, **The Narrow Way Newsletter**, **The Sacred Name Broadcaster**, **The Sacred Name Broadcast**, **The Sacred Scriptures**, **The Sacred Name Telecast**, and **WMLK Radio** are Service Marks and Trademarks of Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507*

***March 2026***
***Volume LVII, Number 12***


# YALIYOMO











***1*   *Mathibitisho 12 yasiyo na Makosa***
*Umuhimu na mpangilio wa siku wakati wa sikukuu za majira ya kuchipua- Pasaka na Sikukuu ya Mikate isiyotiwa Chachu-limekuwa jambo la ubishi miongoni mwa wale wanaoshika siku takatifu za kila mwaka za Yahweh. Watu wa Yahweh wamepewa maelekezo kuhusu wakati ambapo tutaadhimisha ukumbusho wa mateso na kifo cha Yahshua Messiah. Je, utafuata maagizo yaliyomo ndani ya Neno la Yahweh?*

***14*   *Alama ya Mikate Isiyotiwa Chachu***
*Ni nini tafsiri ya kimaandiko ya chachu? Chachu huharibu na kuoza; kwa hivyo, tunajifunza kwamba chachu inawakilisha ushawishi mbaya katika maisha yetu. Inatufanya tuwe wachafu kimaadili na daima itakua tusipoing'oa. Chachu ya mafundisho ya uwongo itatuongoza kwenye dhambi na haitatuongoza katika njia ya Njia Nyembamba ambayo Mwenye-nguvu ametuelekeza tuenende.*

***17*   *Mapishi***
*Sikukuu ya mikate Isiyotiwa Chachu ni wakati wa pekee sana wa mwaka! Yahweh ametupa vyakula vitamu, vilivyo safi, visivyotiwa chachu ili tule ambavyo havina chachu.*



Mtangazaji wa Jina Takatifu huchapishwa kila mwezi na Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507. Uandikishaji wako umelipwa na watendakazi wenza wenye hiari wa huduma hii ambao wanajali kwamba ujumbe huu wa wokovu unapaswa kutolewa bila malipo kwa ulimwengu wote kama shahidi kabla ya Ujio wa Pili wa Yahshua Masihi. Ingawa hakuna malipo yoyote yatakayotozwa kwenye chapisho hili, MICHANGO (yote inakatwa kodi) inakubaliwa kwa shukrani ili kusaidia kulipia gharama. Tunatumahi kuwa utashiriki katika kufanya habari hii ipatikane kwa wengine.

Nukuu zote katika The Sacred Name Broadcaster zimetolewa kwa The Sacred Scriptures, Bethel Edition, 1981, Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507, isipokuwa ikitangazwa vingenevyo. Tafsiri zote za Biblia humu, zimesahihishwa ziwe thabiti na maandishi yaliyo ya awali zaidi yanayopatikana. Nakala za The Sacred Scriptures, Bethl Edition, zinapatikana. Kwa ujumbe jinsi ya kununua kopi yako, andika kwa Assemblies of Yahweh.



© Hakimiliki 2026 Assemblies of Yahweh. Haki zote zimehifadhiwa.



Malipo ya posta ya mara kwa mara huko Reading, PA 19612 (ISSN 879320). Simu (717) 933-4518. POSTA: Tuma fomu 3579 kwa Assemblies of Yahweh, SLP C, Bethel, PA 19507.

***Mwanzilishi na Mwandishi:** Mzee Jacob O. Meyer*


## Jalada Letu

*Mkanda wa kutikiswa dhidi ya anga tulivu unatukumbusha kuhusu Yahshua Aliye Messiah akitimiza sadaka ya malimbuko masaa tu baada ya ufufuo wake. Tunaamini hii ndiyo kwa nini Miriamu Magdalena alidhania kwamba yeye alikuwa Mtunza bustani wa shamba la kaburi- kwa sababu alikuwa amebeba mkanda wa kutikiswa uliokatwa hivi karibuni wa shayiri. **"Yahshua akamwambia, Mama, unalilia nini? Unamtafuta nani? Naye, huku akidhania ya kuwa ni mtunza bustani, akamwambia, mkuu, ikiwa umemchukua wewe, uniambie ulipomweka, nami nitamwondoa. Yahshua akamwambia, Mariamu. Yeye akageuka, akamwambia kwa Kiebrania, Raboni; ambayo ni kusema, mwalimu."** (Yohana 20:15-16).*

*Yahshua kisha alipaa Juu kujiwasilisha Mwenyewe kwa Baba Yahweh katika hali iliyotakaswa. **"Yahshua akamwambia, Usinishike; kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba: Lakini enenda kwa ndugu zangu ukawaambie, ninapaa kwenda kwa Baba yangu naye ni Baba yenu, kwa Elohim wangu naye ni Elohim wenu."** (Yohana 20:17).*




*Yahshua alikuwa binadamu pekee aliyekufa na kufufuliwa tena kuwa kiumbe wa kiroho. Kupitia kwa Yahshua Messiah, ikiwa tumebatizwa kwenye Jina Lake na kubaki waaminifu hadi mwisho, tutapewa maisha ya milele katika ufufua wa wenye haki. (Ufunuo 20:6)*

***"Lakini sasa Messiah amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala. Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhalika na kiyama ya wafu ililetwa na mtu. Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Messiah wote watahuishwa. Lakini kila mmoja mahali pake; limbuko ni Messiah; baadaye walio wake Messiah, atakapokuja."*** *(1 Wakorintho 15:20-23).*

*Ayubu anauliza swali, **"Mtu akifa, je! Atakuwa hai tena?"** (Ayubu 14:14a). Tuna tumaini hii katika ujio wa Pili wa Yahshua. **"Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini. Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yahshua alikufa na kufufuka hata na wao waliolala katika Yahshua, Elohim atawaleta pamoja naye."** (1 Wathesalonike 4:13-14).*

***"Nanyi jiwekeni tayari, kwa kuwa saa msiyodhani ndipo ajapo Mwana wa Adamu."*** *(Luka 12:40)*




# Mathibitisho 12 Yasiyo na Makosa

na Mzee Jacob O. Meyer

Hebu tuchukue **Taarifa ya mafundisho** ya Assemblies of Yahweh na tufungue ukurasa wa 4 (katika toleo la mfukoni), ambapo tunasoma pointi ya 13, 14 na 15.

**Pointi ya 13**: "Tunathibitisha kwamba Ukumbusho wa Chajio cha Pasaka katika kipindi hiki cha Agano Jipya ni maadhimisho ya kila mwaka ya kifo cha Mwokozi wetu. Kumbukumbu ya pasaka ni ya kuangaziwa jioni ya siku ya 14 ya mwezi wa Maandiko wa Abibu, punde tu baada ya machweo, katika mwanzo wa siku, Kutoka 12:3-14; Hesabu 28:16; 1 Wakorintho 5:7-8; 1 Wakorintho 11:23."

**Pointi ya 14:** "Maadhimisho ya Pasaka hutumia nembo zenye zitatumika katika enzi hii ya Agano Jipya. Mkate usiotiwa chachu (matzoth) ni ishara ya mwili wa mwokozi wetu uliovunjwa, 1 Wakorintho 10:16; Kutoka 23:18. Ishara ya damu ya mwokozi wetu iliyomwagika inaeleweka kuwa matunda ya mzabibu. (Kiebrania, *Tirosh* 'asis-grape juice-maji ya zabibu), Mathayo 26:27-29; Isaya 65:8-9; Kumbukumbu ya Torati 32:14; Tunapata kwamba siku ya pasaka yahimiza kutumia kwa mkate usiotiwa chachu, lakini siku hii sio sabato ya kupumzika, Kumbukumbu la Torati 16:3-4. Ni maandalizi kwa ajili ya sikukuu, siku iliyo kabla ya sabato ya mwaka, Mariko 15:42; Luka 23:54, Yohana 19:31, 42; Kutoka 12:18; Kutoka 34:25. Kuoshwa kwa miguu hutangulia kabla ya kula na kunywa nembo hizo, Yohana 13."

**Pointi ya 15**: "Tunathibitisha kwamba Sikukuu ya Mikate isiyotiwa Chachu inatunzwa kutoka siku ya 15 hadi siku ya 21 (siku ya 21 ikihesabiwa) ya mwezi wa Abibu; wakati wa kipindi hiki, tunakula mikate isiyotiwa chachu pamoja na chakula chetu, Walawi 23:6, huku kwa mfano huu tukijitakasa kwa kuondoa chochote kilicho na chachu, yaani mafundisho ya uongo (false doctrine) ambayo yanatuingiza katika dhambi, 1 Wakorintho 5:6-8; Mathayo 16:12; Mariko 8:14-15; Luka 12:1. Siku ya kwanza na ya mwisho ya maadhimisho haya ni ya kutunzwa kama sabato takatifu

na makusanyiko ya kuabudu na kumhimidi Baba wetu wa Mbinguni, Kutoka 12:15-20; Hesabu 28:17-25; Matendo ya Mitume 20:6-7."

Kuna **maneno kadhaa muhimu** ambayo mara kwa mara tunatumia na ambayo yanaongoza Assemblies of Yahweh katika mafundisho safi ambayo yanafanya shirika hili la kipekee miongoni mwa umati wa mashirika ya kidini. Miongoni mwa maneno haya yanayohusiana kwa utafiti wa kina wa Biblia ni **"muktadha**," au "**uwekaji muktadha**," "**kuoanisha**, na "**kusawasisha**." Umeweza pengine kusikia mwandishi akitumia neno "kuoanisha" karibu mara mamia, hasa kama unasikiliza mara kwa mara kwa **The Sacred Name Broadcaster**, au kama umekuwa mwanafunzi katika Obadiah School of the Bible. Bila shaka, utanisikia nikitaja kiuhalisia mara mia zaidi, kabla ya Ujio wa mara ya Pili wa Messiah. "*Kuoanisha Biblia kutoka Mwanzo hadi ufunuo, kufanya kitengo kimoja kamili,*" ndiyo ninayotangaza kwa, matangazo mengi ya radio na katika madarasa mengi ya Obadiah kwa sababu ni hoja ambayo inahitaji kuendeshwa nyumbani.

"*Kutengeneza kitengo kimoja kamili*," ni neno lingine muhimu tunalosisitiza mara kwa mara kwa sababu neno "kitengo" linahusiana kwa neno "umoja."

Kama nomino, *usawa,* linamaanisha *tu kwamba ni lazima tudumishe msimamo wetu, tukisimama sawasawa na kila neno la Yahweh.* Kuishi kwa kila neno la Yahweh (Mathayo 4:4) inamaanisha kamwe tusiwe na msimamo mkali- ama katika mwelekeo huria, au ushupavu mgumu na usio na busara- kihafidhina zaidi- katika upande mwingine. Lazima tuichukue Biblia katika muktadha, kuiruhusu kuoana kote kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, kuichukulia kama jumla ya nyenzo la umoja na kudumisha usawa wetu kwa kila neno.

Kuna maendeleo ambayo wakati mwingine hutoka katika utawala wa Assemblies of Yahweh ambayo yanatoa kwetu sababu kwa mshangao mkubwa. Wakati mshiriki wa Assemblies of Yahweh anageuka kando katika mafundisho ya uongo baada ya kuwa katika Imani kwa miaka kadhaa, mtu anashangaa juu ya uaminifu wake wa awali.

Kwa nini inatokea? Hivi majuzi, nilianza kutazama kipindi cha televisheni, ambacho hakikunivutia sana baadaye, hivyo nikaenda kulala, lakini mzungumzaji alianzisha programu kwa kuashiria kwamba mambo ya ajabu yanafanyika duniani katika mwanzo wa kila mwongo. Lakini hapa tuko katika mwanzo wa mwongo wa mwisho katika karne ya mwisho ya milenia hii na, pengine, matukio yanakuwa ya kutatanisha- geni na mageni. Ninaweza kukubaliana kwa moyo wote na uchunguzi kama huo. Kwa nini mtu anaondoka kutoka kwa Imani? Je, hatujaonywa kuhusu anguko kubwa kutoka kwa Imani *(apostasia*) katika 2 Wathesalonike 2:4?

Hapa tunapendekeza baadhi ya suluhisho kwa fumbo hili: a) kusahau yale waliyojifunza- kwa maneno mengine, kusahau kuhakiki; b) kusahau kusoma Biblia- hilo ni kupuuza; c) kusoma maandishi mengine ya kidini bila uhakiki- hilo linamaanisha kuendeleza unyonge, na d). Kusahau kuichukulia Biblia kama kitengo kimoja kamili- kutooanisha nakala.

Kanuni hii inajadiliwa katika **Maagizo katika Ahadi ya Agano**, ambayo wazee wa Assemblies of Yahweh wanaelezea kila wakati tunashauri mtu kwa ubatizo. **Maagizo katika Ahadi kwa Agano**, pointi ya 3 na 4, zinasoma: *"3. Uaminifu wako sasa ni kwa Assemblies of Yahweh kama Mwili wa pekee wa kweli wa Messiah.* [Isipokuwa, naweza kuongezea kwa mabano, wewe ni Anania na Safira (Matendo 5:1-11).] *Ni lazima uwe tayari kufanya-kazi ndani ya mwili huo, Waefeso 4:1-7; Kutoka 13:18; Hesabu 10:3; Yohana 15:4.*

*"4. Unapokumbana na matatizo juu ya mafundisho, kwa upinzani wa wengine, au ukifikiria kwamba umepata nuru mpya, usiende kwa wengine ili upate maelezo, bali nenda kwa Wazee wa Assemblies of Yahweh. Lazima uwe tayari kupokea marekebisho kutoka kwa wazee wa Assemblies of Yahweh juu ya fundisho lolote linalohusika, Waefeso 4:11-14; Tito 1:9-10; 1 Petro 5:1-6; Waebrania 13:7, 17; Kumbukumbu la Torati 17:2-13; Hesabu 11:17, 25,"*

Katika toleo la mfukoni la **Taarifa ya Mafundisho**, katika ukurasa wa 7, aya mbili za kwanza zinasema: "*Maswala ya kimafundisho ya makusanyiko yote yatawekwa mipaka na kuwa katika himaya ya askofu na watumishi walioteuliwa. Ikiwa mshiriki ana matatizo yoyote na mafundisho, anatakiwa kuandika muhtasari wa imani yake na auwasilishe kwa kamati ya kudumu ya mapitio ya mafundisho* [ambayo ni wazee walioteuliwa, tunaelezea kwa mabano]. *Maamuzi ya kimafundisho lazima yafanywe na wazee wenye kuhubiri (preaching eldership), kulingana na Matendo ya Mitume 15 [ambayo inatupa mfano wa jinsi mambo ya mafundisho yalizingatiwa, kuhukumiwa, na kueleweka katika Kusanyiko la kitume], na sio katika kusanyiko la jumla. Washiriki wote katika Assemblies of Yahweh watalingana na 1 Wakorintho 1:10 na Waefeso 4:1-7, katika umoja wa kimafundisho. Assemblies of*




***Shirika la Assemblies of Yahweh litaendelea kwenda katika mwelekeo wa kweli wa maelewano na Maandiko Matakatifu.***

*Yahweh lazima itunzwe kama mwili mmoja, kufuata mfano wa 2Wathesalonike 3:6-16...."*

Wakati mshiriki anaanza kusambaza maandishi yaliyo na mafundisho ya uongo, hakuna mbadala kwetu isipokuwa kuchukua hatua ya mara moja. Mzee wa Kuongoza aliifanya katika siku zilizopita, na nitafanya hivyo katika siku zijazo. Je, tutakuwa katika umoja wa kimafundisho, au tutaendelea katika Babeli (mkanganyiko) kama vile Ukr-sto unavyofanya, na kama inavyoonekana, zinavyofanya dini zote leo? Je, tutaendelea kubaki ndani na kushiriki katika Babeli ya kimafundisho ambayo imechujwa kwa chachu, ambayo imeharibiwa na kudhoofishwa na mafundisho ya uwongo na dhambi, au tutabakia katika umoja wa kimafundisho- walio na nguvu katika Imani, wanaoweza kushika upanga wenye makali kuwili wa neno la Yahweh kwa njia yake yenye matokeo zaidi? Kumbukadhambi ni uvunjaji wa Shera za Yahweh (1 Yohana 3:4). Jibu, bila shaka, ni hatua ya mwisho: **lazima tubaki katika umoja wa mafundisho**.

*"Uhubiri wa mafundisho safi lazima utunzwe; kwa hivyo, watumishi tu ambao wameteuliwa, wenye ujuzi au wanaume wanaofunzwa na Assemblies of Yahweh wataruhusiwa kuhubiri au kupata nafasi kwenye jukwaa, kwa swala hili. Mtumishi wa cheo cha juu anayeabudu katika mkutano fulani wa Assemblies of Yahweh, atahuburi ujumbe mkuu, wakati huo. Huduma ya Sabato ya mara kwa mara itakuwa na mahubiri fupi ya hiari na mahubiri kuu, kwani maandiko hayatambui shule ya sabato (Sabbath school)."*

Hakuna walimu katika Assemblies of Yahweh isipokuwa wale ambao wameteuliwa. Mtu anapojitwika jukumu la kufundisha, mtume Yakobo anasema, basi kusiwe na walimu wengi, maana ndio watapokea hukumu nzito zaidi (Yakobo 3:10). Kwa hivyo, hakuna mtu anayepaswa kufundisha chochote katika Assemblies of Yahweh **isipokuwa wale walioteuliwa na shirika kufundisha.**

Wakati fulani watu hupata matatizo ya kiroho kwa sababu wanaanza kujiona wenyewe kama walimu. Sisi sote lazima tuwe wanafunzi, kwanza na kimsingi. Neno ambalo linatokana na neno la Kiebrania *limmud* linalomaanisha *kujifunza*. Tazama # 3928 katika **Strong's Exhaustive Concordance of the Bible**. Sote tunapaswa kuwa wanafunzi, na wachache sana wanapaswa kuwa walimu. Hii ni kwa maelekezo ya uongozi wa Baraza la Mitume wa awali- Yakobo, ndugu wa Yahshua mwenyewe wa nyama na damu.

Wakati mwingine watu wanaendeleza matatizo na ufahamu wa Pasaka na Sikukuu ya Mkate usiotiwa chachu, ambayo ni mada ya nakala hii. Bila kujivunia, lazima niseme kwamba nimesoma somo hili kwa undani. Kamwe sitabadilisha fundisho hili kutoka kwa yale ambayo tumechapisha katika maandishi ya Assemblies of Yahweh, haswa **Taarifa ya Mafundisho**. Shirika la Assemblies of Yahweh litaendelea kwenda katika mwelekeo wa kweli wa maelewano na Maandiko Matakatifu.

Uthibitisho usio na makosa hujitokeza **tunapooanisha** Neno la Yahweh. Niliketi chini hivi majuzi, kwa dakika chache tu, na kuandika zaidi ya **Mathibitisho 20** yasiyo na makosa ambayo **hayawezi kukanushwa.** Tunapaswa kutegemea mawazo na utafsiri wa mashirika mengine

***Yahshua aliye Messiah alikuja kurejesha Ibada ya kweli kwa Uyahudi, kwa kufundisha mafundisho safi ya Neno lililoandikwa la Yahweh. Kwa nakala hii, ni matumaini yangu kumshawishi mtafutaji wa Kweli kwa mafundisho safi ya Biblia.***

ya kidini? Ndugu, angalieni kwa makini kwamba mnashikamana kikamilifu na **Torati iliyoandikwa** na si kwa tafsiri za sheria ya Kiyahudi ya mdomo, ambazo HATUKUBALI kuwa zimevuviwa.

Wakati mwingine watu watasoma maandishi bila uhakiki. Au wakati mwingine watu hufikiri kwamba kwa kuwa Uyahudi unatii sehemu kubwa ya sheria ya Maandiko, watakuwa wakifundisha KWELI YOTE. Baadhi ya watu wanaamini kwamba ni lazima tuyabane mafundisho ya Agano Jipya katika ufasiri wa Torati ya mdomo ya Kiyahudi, jambo ambalo si kweli. Hebu tuangalie baadhi ya vifungu ambavyo vitakanusha dhana hizo.

Angalia kama utangulizi, Mathayo 15:3, ***"Akajibu, akawaambia, Mbona ninyi nanyi huihalifu amri ya Elohim kwa ajili ya mapokeo yenu?"*** Mwandishi anaweza kukuelekeza kwa vifungu katika Mishna na katika Talmud (Sheria za Mdomo), na ninaweza kuashiria matukio mengi ambapo maamuzi ya kirabi yamepingana kwa wazi na amri zilizoandikwa za Torati. Utachukua mwelekeo upi? Assemblies of Yahweh itafuata mafundisho ya Messiah, kwa sababu tutashikamana kabisa kwa Torati iliyoandikwa (sheria). Yahshua anasema katika mstari wa 6, ***"Na mmelitangua*** [KUKIUKA] ***neno la Elohim kwa ajili ya mapokeo yenu."*** Mafundisho ya kirabi (maamuzi ya kirabi) ndiyo yanayojulikana kama mila za wazee.

Mathayo 15:12-14 inasoma, ***"Ndipo wanafunzi wake walipomwendea, wakamwambia, wajua ya kuwa Mafarisayo walipolisikia neno lile walichukizwa? Akajibu, akasema, Kila pando asilolipanda Baba yangu wa mbinguni litang'olewa. Waacheni; hao ni viongozi vipofu, Na kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, watatumbukia shimoni wote wawili."*** Tunaliona hilo waziwazi kwamba Yahshua aliye Messiah hakuwa mwanadiplomasia, lakini alisema (kwa kufafanua), *"Sijali kuhusu mtazamo wa Mafarisayo; lazima niwajibike kwa uaminifu kwa Mwenye-nguvu Yahweh na kwa neno lililoandikwa."*

Mwandishi anasema jambo sawa kabisa leo, ***"Na kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, watatumbukia shimoni wote wawili."*** (Mathayo 15:14). Tafadhali angalia pia ungwaji mkono wa Messiah kwa Torati iliyoandikwa. (Mathayo 5:17-20).

Mariko mlango wa 7 una simulizi sambamba kwa yale yaliyofanyika. ***"Basi wale Mafarisayo na waandishi wakamwuliza, mbona wanafunzi wako hawaendi kwa kuyafuata mapokeo ya wazee, bali hula chakula kwa mikono najisi? Akawaambia, Isaya alitabiri vema juu yenu ninyi wanafiki, kama ilivyoandikwa, Watu hawa huniheshimu kwa mdomo, ila mioyo yao iko mbali nami. Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu***

***"Ninyi mwaiacha amri ya Elohim, na kuyashika mapokeo ya wanadamu. Akawaambia, Vema! Mwaikataa amri ya Elohim mpate kuyashika mapokeo yenu…Huku mkilitangua neno la Elohim*** [Yahweh] ***kwa mapokeo yenu mliyopokeana; tena mwafanya mambo mengi yaliyo sawasawa na hayo."*** (Mariko 7:5-9, 13).

Sihimizi kusoma maandishi kutoka kwa mashirika mengine ya kidini. Ninahimiza usomaji wa mara kwa mara wa Biblia na kusoma mafundisho safi yanayoelezewa na maandishi ya Assemblies of Yahweh. Lakini, kama mtu atasukuma kitu cha maandishi mikononi mwako, au kama utasoma maandishi yoyote mengine kuliko yale tunachapisha, unapaswa kufanya hivyo kwa umakini, badala ya kumeza tu aina yote ya dhana ambazo hazithibitishwi kutoka kwa Biblia. Ningekubaliana na yale aliyosema Yahshua aliye Messiah. Basi utambue kwamba Uyahudi hauna Ukweli wote. Hawakubali Jina Takatifu **Yahweh**; hawatunzi siku takatifu ipasavyo; na hawafundishi ufahamu sahihi wa maisha baada ya kifo. (Wengi katika Uyahudi wanashikilia fundisho la kuzaliwa upya katika mwili, ambalo ni fundisho lisiloweza kuungwa mkono katika mtazamo wa Mhubiri 9:2-6.)

Nakusudia kuleta *uthibitisho 12 usio na makosa,* kati ya thibitisho thabiti zaidi kwamba njia ambayo mafundisho yanasemwa kwa ufupi na kuonyeshwa katika **Taarifa ya Mafundisho** ya Assemblies of Yahweh ni sahihi

***'Na ile damu itakuwa ishara kwenu katika zile nyumba mtakazokuwamo; nami nitakapoiona ile damu, NITAPITA JUU YENU, na hakutakuwa na pigo lolote litakalowaharibu, nitakapoipiga nchi ya Misri."***

(KUTOKA 12:13)



kweli. Nitaiweka wazi sana kupitia masomo haya kwamba **Taarifa ya Mafundisho** ya Assemblies of Yahweh ni hati sahihi sana, ya ukweli, na iliyosomwa vyema. Uthibitisho huu 12 uliotolewa katika nakala hii unathibitisha kwamba Assemblies of Yahweh inashika Pasaka ipasavyo.

## UTHIBITISHO 1

Neno *Pasaka* linamaanisha hilo hasa, *kupita juu*. Siku hiyo ilitoa jina lake kwa mwana-kondoo wa *Paschal*, au dhabihu, SI KINYUME CHAKE. Katika **Webster New World Dictionary, Second College Edition**, tunaona kwamba hata watu wa kilimwengu wanaelewa Ukweli huu. "*Pasaka [PASS+OVER, iliyotumiwa kutafsiri Pesah ya Kiebrania: tazama PASCH] 1. Sikukuu ya Kiyahudi [badala yake sema sikukuu ya kimaandiko] (pesach) iliyoadhimishwa kwa siku nane (au saba) kuanzia siku ya 14 ya Nisani na kuadhimisha ukombozi wa Waebrania wa kale kutoka utumwani katika Misri: Kutoka 12. 2. [p-] zamani, mwana-kondoo wa paschal."*

Kwa nini ufafanuzi huo ni *sahihi jinsi* uwezavyo na kuwa katika maelewano kabisa na Biblia! Kufuatia ufafanuzi huu, wahariri wanatoa marejeleo ya Kutoka sura ya 12.

Hebu tugeukie mara moja kwenye Kutoka sura ya 12. Kuanzia mstari wa kwanza tunasoma, ***"Yahweh akanena na Musa na Haruni katika nchi ya Misri, akawaambia, Mwezi huu utakuwa mwanzo wa miezi kwenu; utakuwa ni mwezi wa kwanza wa mwaka kwenu."*** (Kutoka12:1-2).1Wayahudi bila shaka wanabainisha kwamba Rosh Hoshana ni kichwa cha mwaka. Siku ya kwanza ya mwezi wa saba katika msimu wa majani kupukutika inaitwa Mwaka mpya wa Kiyahudi, (*Rosh Hoshana, maana yake ni kichwa cha mwaka*).

Katika jarida la **Israel** (Septemba 1971) katika nakala yenye kichwa, "**Did you know That**…?" Mwandishi, Rabbi Shmuel Avidor Hacohen, anauliza swali "*Kwa nini tunaweka Rosh Hoshana kwa majira ya kupukutika ya mwaka wakati Biblia inasema ni majira ya machipuo ya mwaka?"* Naam, hilo ni swali nzuri. Sihitaji kujibu swali- mamlaka ya Uyahudi lazima yalijibu.

Assemblies of Yahweh hawaiti siku ya kwanza ya mwezi wa saba Rosh Hoshana. Tunaiita sikukuu ya baraghumu, na ndivyo inavyostahili, kama Maandiko Matakatifu yanavyofanya.

***"Semeni na mkutano wote wa Israeli, mkawaambie, siku ya kumi ya mwezi1***[baini hili kwa uangalifu sasa]***huu kila mtu atatwaa*** [au atachagua] ***mwana-kondoo kwa watu wa nyumba moja: na ikiwa watu wa nyumba ni wachache kwa mwana-kondoo, basi yeye na jirani yake aliye karibu na nyumba yake na watwae mwana-kondoo mmoja, kwa kadiri ya hesabu ya watu; kwa***



***...ungeweza kumchukua***

***mwana-kondoo huyu***

***...na kumfanya mnyama kipenzi...***

***Watoto wako wangecheza naye.***

***kadiri ya ulaji wa kila mtu, ndivyo mtakavyofanya hesabu yenu kwa yule mwana-kondoo."*** 1(Kutoka 12:3-4). Ingeweza kuwa familia mbili zinazochagua mwana-kondoo pamoja, au kila familia ya Waisraeli kula kivyake katika nyumba zao za kibinafsi, lakini si kusanyiko (Kiebrania-qahal) lote pamoja. Pasaka katika Misri ilipaswa kuwa maadhimisho ya familia. (Hii ndiyo sababu Assemblies of Yahweh inatenganisha kati ya familia ya Yahweh ambao wamefanya kujitolea kwao kibinafsi kwa Agano la Yahweh na wale ambao wako bado katika *qahal*, kusanyiko la jumla.) *'Edah* (familia ya kiroho, au kutaniko la kiini) huadhimisha Ukumbusho wa Pasaka pamoja. Qahal wanaangalia, au wanabakia nyumbani.

***"Mwana-kondoo wenu atakuwa hana ila, mume wa mwaka mmoja*** [wa mwaka wa kwanza- mwanakondoo mdogo]: ***mtamtwaa katika kondoo au katika mbuzi: Nanyi mtamweka hata*** [Kiebrania- 'ad: kusonga mbele kuelekea, au kusonga hadi- **Holladay Lexicon**] ***siku ya kumi na nne ya mwezi ule ule; na kusanyiko lote la mkutano wa Israeli watamchinja jioni."*** (Kutoka 12:5-6).

Je, hata (Kiebrania- *'ad*) siku ya kumi na nne ya mwezi huohuo ina maana gani? Inamaanisha kuwa hupiti zaidi ya siku ya kumi na nne, lakini unaweka mwana-kondoo wa Pasaka HADI, au siku ya kumi na nne ya mwezi huohuo itakapoanza- uiweke hadi Abibu 14. Ninatumia jina *Abibu* kama mwezi wa kwanza wa kimaandiko badala ya neno *Nisani* kwa sababu imethibitishwa kwamba *Nisani* ni Aliye na Nguvu wa Babeli wa majira ya machipuko. Abibu linamaanisha MASUKE YA KIJANI. Neno *kusanyiko* hapa ni *qahal* katika Kiebrania na neno *congregation* ni *'edah* katika nakala ya Kiebrania. Kwa hiyo, kutaniko la kusanyiko wataweka Pasaka.

***"Nao watatwaa baadhi ya damu yake na kuitia katika miimo miwili na katika kizingiti cha juu, katika zile nyumba watakazomla."*** (Kutoka 12:7). Waisraeli walikuwa nyumbani kwa dhabihu hii ya Pasaka, na kamwe tusisahau ukweli huu. Kila familia binafsi ya Waisraeli ilipaswa kufanya huduma hii usiku sahihi, au kuteseka kifo cha wazaliwa wa kwanza wote, wa wanadamu na wa wanyama, katika nyumba hiyo iliyopuuza.

Watafanya nini? ***"Watakula nyama yake usiku ule ule, imeokwa motoni, pamoja na mkate usiotiwa chachu; tena pamoja na mboga zenye uchungu. Msiile mbichi, wala ya kutokoswa majini, bali imeokwa motoni, kichwa chake pamoja na miguu yake, na nyama zake za ndani."*** (Kutoka 12:8-9). Kwa maneno mengine, Waisraeli hawangefanya chochote kwa mwana-kondoo bali kumkata koo lake, kuteka damu katika beseni, na kisha kuchukua hisopo na kuinyunyuzia damu hiyo kwenye kizingiti cha juu na kwenye miimo ya kando ya milango. Waisraeli walipaswa kubeba mwana-kondoo ndani ya nyumba zao na kumchoma mara moja juu ya moto ulio wazi. Hawangeweza kuondoa ngozi, au kukata kichwa. Hakuna cha ndani ambacho kingeweza kutolewa. Oka kama tu alivyo, Yahweh aliagiza. Unaweza kusema ni sikukuu ya kupendeza? Hakikahaingependeza sana!

Kama ungefuata hasa kwa maelekezo ya Yahweh ambayo alitoa kwa Msua kuwaagiza Israeli, ungeweza kumchukua mwana-kondoo huyu na pengine kumleta ndani ya nyumba kwa zaidi ya siku tatu na kumfanya mnyama kipenzi (katika siku ya 10, 11, 12, na 13). Watoto wako wangecheza naye. Angekuja na kujisugua mwenyewe dhidi ya miguu yako, pengine ulipokuwa unakula chajio.

Kisha, katika mwanzo wa Abibu 14, ungemchukua nje jioni, ungemuua, ukinyunyizia damu kwenye miimo ya mlango na juu ya kizingiti cha nyumba yako, ukaleta mzoga ndani ya nyumba, ukaupachika juu ya moto wazi, na kuoka (mchakato ambao unapaswa kuchukua labda saa moja, au saa moja na nusu). Hukuwa na popote pa kwenda, kwa kuwa uliagizwa ubakie nyuma ya ishara ya damu, kwa hivyo kama mchakato wa kuchoma ulichukua masaa mawili, au hata masaa mawili na nusu,hilo lilikuwa jambo gani? Je, unaweza kuwazia kulazimika kula kitu kama mzoga wa mwana-kondoo huo mara tu baada ya kumchinja?

Kuhusu suala la ulaji mboga, Biblia inasema, "**Watakula nyama**." Hiyo ni amri wazi. **Hiyo ni mitzvah**! Ni amri kutoka kwa mdomo wa Yahweh. YAHWEH SI MLA MBOGA. Hataki tuwe walaji mboga pekee. Tunapata katika Kutoka 12:8 amri ya kula nyama! Kuna maandiko kadhaa ya ziada katika Biblia yanayotuamuru kula nyama. Kama Waisraeli wangekuwa walaji wa mboga pekee(vegeterian), WANGEKUWA BADO KATIKA MISRI! **Hadi siku hii hasa, wangekuwa bado hawajaachiliwa.** Zaidi ya hapo, kuna maneno mawili katika Kiebrania ambayo hutumiwa kwa kuchinja, au kwa kuua. Moja ni *shachat*, ambayo ina maana ya *kuchinja wanyama kwa ajili ya chakula*. Kutoka kwa neno hili linakuja neno *shechitah*, *ambalo linamaanisha kuchinja wanyama kwa chakula*.

Neno lingine ni *ratzach*, ambalo linaonekana katika amri ya sita ya Decalogue (amri 10) likiwa na maana ya *kuchukua uhai wa mwanadamu*. **Yahweh hutofautisha- kwa maneno- kati ya kuua mwanadamu (mauaji) na kuchinja wanyama kwa ajili ya chakula**. Inaweza kuonekana kwangu kwamba mamlaka ya Uyahudi inapaswa kujua ukweli huu na kuufundisha kwa nguvu.

***"Wala msisaze kitu chake chochote hata asubuhi, bali kitu kitakachosalia hata asubuhi mtakichoma kwa moto."*** (Kutoka 12:10), Waisraeli walihitajika kula baadhi ya mwana-kondoo aliyechomwa, lakini Yahweh alijua hawangeweza kumla wote. Lilikuwa ni jambo lisilopendeza sana kwa Waisraeli kumchukua huyo mwana-kondoo mdogo ambaye ulikuwa umetoka tu kumpapasa akiwa hai, wamuue, na kumchoma akiwa na kichwa chake na miguu yake, ili kwamba bado ungeweze kutambua vipengele vyake na, hata akiwa na sufu juu yake, yote yamesawijika na kuungua, na kisha, kuilaza kwenye sinia, kaikata kata, na uile. Yahweh alijua kwamba Waisraeli hawangeweza kula sana, lakini walipaswa kula angalau sehemu yake.

***"Tena mtamla hivi, mtakuwa mmefungwa viuno vyenu, mmevaa viatu vyenu kando ya miguu yenu*** [sio kwenye miguu yenu]***, na fimbo zenu kando ya [sio katika] mikono yenu, nanyi mtamla kwa haraka*** [au hofu]; ***ni pasaka ya Yahweh. Maana nitapita kati ya nchi ya Misri USIKU HUO, nami nitawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri wa mwanadamu na wa mnyama; nami nitafanya hukumu juu ya elohim zote za Misri; mimi NDIMI YAHWEH"*** (Kutoka 12:11-12).

Baini tena mambo tuliyosoma: chagua mwana-kondoo katika siku ya kumi ya mwezi, weka HADI siku ya kumi na nne, na umchinje JIONI HIYO – KATIKA JIONI (mstari wa 6). Weka damu kwenye kizingiti cha juu na miimo ya kando ya mlango wa nyumba ambapo utaoka na kula mwana-kondoo. Kula mwana-kondoo aliyechomwa, mzima. Msimkate, wala usiuvunje mfupa wake wowote. Kwa wazi, pamoja na mkate usiotiwa chachu na mboga chungu, huo ungekuwa mlo wa ukumbusho- si karamu!

Kwa kuwa nilizaliwa na kukulia katika malezi ya kilimo, nakumbuka kuua wanyama shambani. Baba yangu, ambaye ni mkarimu na mwenye moyo mpole kuelekea wanyama- baada ya kuua mnyama, hakutaka kula kwa huyo kwa siku kadhaa, au hata majuma. Sisi watoto, pia, tungekuwa na wakati mgumu kwa kiasi fulani kuanza kula nyama kutoka kwa mnyama huyo. Tulikuwa tumelisha na kumtunza. Tulimuuguza wakati alikuwa mgonjwa. Tulimbebeleza alipotujia. Unafikiri juu ya mambo haya yote wakati unaua mnyama na wakati unamla. Baada ya kumbukumbu ya mnyama inafifia, mambo ni tofauti. Yahweh alikuwa amewaambia Israeli wale mwana-kondoo mara tu baada ya kumchinja.

*"Unapochukua kipande cha nyama kwenye sinia yako, unakula kila kipande chake cha mwisho, kwa sababu mnyama alitoa maisha yake kwamba unaweza kula. Usithubutu kutupa chochote chake."* Siku zote nimewafundisha watoto wangu dhana hii. Yahweh aliwaagiza Waisraeli wamle mwana-kondoo wote. Lakini bila shaka Yeye alijua kwamba hili litakuwa

***Pasaka imepangwa na Mwenye-nguvu Yahweh kwa siku ya 14 ya Abibu na Sikukuu ni ya kuangaliwa kutoka siku ya 15 ya mwezi na inaenda kupitia siku ya 21 ya Abibu. Hakuna mwanadamu anaweza kubadilisha tarehe hii kwa njia yoyote. Hili ndilo Biblia inavyosema.***

amri ngumu kutimiza, hivyo aliwatolea mbadala. Amri ya Yahweh iliwaamuru Israeli wasiondoke kwa nyumba zao kabisa usiku huo. Hawangeacha nyumba zao, au wangeacha ulinzi wa damu na kufa. Asubuhi walikuwa wachome mabaki ya mwana-kondoo, kwa sababu wangeenda nje tena. Kuchoma mabaki ya mwana-kondoo ingechukua wakati fulani.

***"Na ile damu itakuwa ishara kwenu katika zile nyumba mtakazokuwamo; nami nitakapoiona ile damu, nitapita juu yenu, na hakutakuwa na pigo lolote litakalowaharibu, nitakapoipiga nchi ya Misri."*** (Kutoka 12:13). Hapa ndipo neno *Pesach*, au Pasaka, linaingilia. *Pesach* linamaanisha *kuruka, kuruka juu, na kuachiliwa* (**Strong Concordance,** #6452). Musa aliwaambia Israeli "*Kaeni ndani ya nyumba; msitoke nje kwa sababu mtahatayarisha wokovu wenu mkifanya hivyo. Damu italinda, lakini Israeli alihitajika kukaa ndani ya ulinzi huo."*

Kuanzia katika mstari wa 28 tunasoma, ***"Basi wana wa Israeli wakaenda na kufanya mambo hayo; vile vile kama Yahweh alivyowaamuru Musa na Haruni, ndivyo walivyofanya.***

***"Hata ikawa, USIKU WA MANANE ,Yahweh akawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri, tangu mzaliwa wa kwanza wa Farao aliyeketi katika kiti chake cha enzi, hata mzaliwa wa kwanza wa mtu aliyefungwa katika nyumba ya wafungwa na wazaliwa wa kwanza wote wa wanyama. Farao akaondoka usiku, yeye na watumishi wake wote, na Wamisri wote, pakawa na kilio kikuu katika Misri; maana hapakuwa na nyumba hata moja asimokufa mtu. Akawaita Musa na Haruni usiku, akasema, ondokeni tokeni katika watu wangu, ninyi na wana wa Israeli; enendeni, kamtumikieni Yahweh kama mlivyosema."***1(Kutoka 12:28-31).

Je, Musa na Haruni walienda nje mara moja? Sio kabla ya macheo ya jua, hawakuenda (maana ya neno la Kiebrania *boqer* ni *macheo ya jua*). Farao aliwatuma watumishi wake, na iliwabidi kusafiri hadi Gosheni ambapo Israeli walikaa. Hili lilichukua wakati fulani.

***"Wamisri nao wakawahimiza watu, kuwatoa katika nchi haraka, maana walisema, tumekwisha kufa sote. Watu wakauchukua unga wa mikate yao kabla haujatiwa chachu, na vyombo vyao vya kukandia wakavitia ndani ya nguo zao mabegani. Wana wa Israeli wakafanya kama neno lile la Musa, wakataka kwa Wamisri vyombo vya fedha na vyombo vya dhahabu, na mavazi. Yahweh akawajalia kupendelewa na Wamisri hata wakawapa kila walichokitaka. Nao wakawateka nyara*** [kuwanyang'anya]***Wamisri.***

***"Wana wa Israeli wakasafiri kutoka Ramesesi mpaka Sukothi, walipata hesabu yao kama watu sita mia elfu watu waume waliokwenda kwa miguu, bila kuhesabu watoto"*** (Kutoka 12:33-37). Na muktadha unasoma katika mstari wa 42, kwamba ni usiku wa kuangaliwa sana kwa Yahweh KWA KUWATOA KUTOKA NCHI YA MISRI. ***"...Huu ndio usiku wa Yahweh, ambao wapaswa kuangaliwa sana [kusherehekewa] na wana wote wa Israeli wote katika vizazi vyao..."*** Nini umuhimu wa istilahi***"kwa sababu ya kuwatoa katika nchi ya Misri"*** ?

**Ilibidi Israeli wasafiri kutoka Gosheni hadi Ramesesi kuja pamoja katika mwili uliounganishwa–katika kusanyiko ukipenda-kutoka katika Misri.** Hivyo nini walipaswa kufanya kabla ya kuondoka? Walipaswa kuuchoma mwili wa mwana-kondoo. Walikuwa wawateke nyara Wamisri. Walipaswa kukusanya mali yao, ambayo walikuwa wamepakia katika nyumba zao. Walipaswa kusafiri hadi Ramesesi.

Ni kwa urefu wa muda upi unafikiria kumalizia kazi hizi zote ungechukua? Jibu ni, mabaki ya siku ya 14 ya Abibu!

Siku ya Pasaka, ilikuwa imetolewa kwao, bila shaka, KWA SABABU HAWANGEENDA NJE YA MILANGO MPAKA BOQER, AMBAYO NI ASUBUHI (MACHEO), au damu ya mwana-kondoo haingeweza kuendelea

kuwalinda wao.

Israeli waliishi wapi? Kutoka 8:22 inasema, ***"Nami siku hiyo nitatenga nchi ya Gosheni, WATU WANGU WANAYOKAA, ili hao mainzi wasiwe huko, ili kwamba upate kujua wewe ya kuwa mimi ndimi Yahweh kati ya dunia. Nami nitatia MPAKA KATI YA WATU WANGU NA WATU WAKO; ishara hiyo italetwa kesho."*** (Kutoka 8:22-23.) Mpaka ulikuwa wapi? Ulikuwa KATI YA GOSHENI NA MABAKI YA MISRI. Zaidi ya hapo, lazima tukumbuke kwamba zaidi ya Waisraeli milioni mbili waliishi katika Gosheni na, pamoja na umati mchanganyiko (Kutoka 12:37), hawa walipaswa KUSAFIRI HADI MAHALI PA KATIKATI PA MKUTANO, kuondoka Misri katika njia yenye mpango- na usimamizi fulani wa usafiri! Musa alikuwa mratibu bora wa umati mkubwa wa watu!

## UTHIBITISHO 2

Siku zote, Pasaka imeainishwa kuadhimishwa tarehe 14 ya Abibu, ikimaanisha siku maalum ya saa 24 ya Abibu. Siku ya kimaandiko inaanza na kuishia machweo. (Walawi 23:32 na Mariko 1:32). Katika Mwanzo 1:5, Kiebrania inasoma, *"wayehi- 'ereb wayehi- boqer yom echad."* Na huwezi kubadilisha mipaka ya siku hiyo ya saa 24.

Hebu tugeukie kwa Walawi 23:4 ambapo tunasoma, ***"Sikukuu [Kiebrania-** moedim**] za Yahweh ni hizi, ni makusanyiko matakatifu, ambayo mtayapigia mbiu kwa nyakati zake. Mwezi wa kwanza, siku ya kumi na nne ya mwezi wakati wa jioni, ni pasaka ya Yahweh. Na siku ya kumi na tano ya mwezi ule ule ni sikukuu kwa Yahweh ya mkate usiotiwa chachu; mtaila mikate isiyochachwa muda wa siku saba. Siku ya kwanza mtakuwa na kusanyiko takatifu: msifanye kazi yoyote ya utumishi. Lakini mtasongeza sadaka kwa Yahweh kwa njia ya moto siku saba; siku ya saba ni kusanyiko takatifu; msifanye kazi yoyote ya utumishi."*** (Walawi 23:4-8).

Kifungu hiki kwa wazi kinatuelekeza kwamba Pasaka imepangwa na Mwenye-nguvu Yahweh kwa siku ya 14 ya Abibu na Sikukuu ni ya kuangaliwa kutoka siku ya 15 ya mwezi na inaenda kupitia siku ya 21 ya Abibu. Hakuna mwanadamu anaweza kubadilisha tarehe hii kwa njia yoyote. Hili ndilo Biblia inavyosema.

Kifungu hapa katika Walawi 23:5 kinasema katika Kiebrania, *"beyn ha'arbayim pesach leYahweh" (katika jioni ni Pasaka ya Yahweh)*. Ni Pasaka ya Yahweh, ambayo ni ya kuanzia katika *beyn ha' arbayim*. Neno hilo linatafsiriwa "jioni." Na kisha, kupitia juu kwa nyumba za Waisraeli kutatokea katika usiku wa manane wa siku hiyo, kipindi sawa cha wakati cha masaa 24

## UTHIBITISHO 3

Nitazingatia kwa ufupi juu ya neno *beyn ha'arbayim*, kutoka kwa wingi wa leksimu na sarufi, pamoja na **Strong's Concorance**, #977, tunapata kwamba *beyn* ni kihusishi. Mzizi wa *ha' arbayim* ni neno *'ereb*, kumaanisha *jioni* au *dusk*. **Holladay's Hebrew**

***Tunapaswa kuzingatia kwamba katika jioni ni wakati Haruni aliwasha taa, sio baada ya jua kupita kilele chake baada tu ya saa sita. Hilo ndilo beyn ha'arbayim linamaanisha, katika jioni wakati taa ziliwashwa. Wakati alichoma uvumba (asubuhi), alitayarisha taa kwa ajili ya kuwashwa jioni, wakati alianza kuchoma uvumba. Ni jambo la kudumu mbele za Yahweh.***



**Lexicon** inatuarifu kwamba neno *beny ha'arebayim* linamaanisha JIONI. Katika **Strong's Concordance** #6148 hadi 6159 kila moja inafafanua tofauti ya neno *ayin, resh, beth*, na zote zinatafsiriwa mbalimbali hadi kwa neno *'ereb*, linalotolewa kama *raven (kunguru)*, ambaye tunaijua ni ndege mweusi. Kutoka kwa neno hili inakuja istilahi *'oreb* ambalo ilikuwa jina la mmoja wa wafalme wa mashariki. Nambari #6159 katika **Strong's Concordance**, *ereb*, inatafsiriwa tena kama *dusk (jioni)*. Kutoka kwa neno hili inakuja tafsiri, *watu waliochanganyika* na jina la kabila linaloitwa Waarabu, maana yake *watu wa rangi dusky* (Kutoka 12:38).


Wayahudi wana ile wanayoita huduma ya *Mincah*, ibada ya alasiri ya sinagogi, na ibada ya jioni ambayo wanaita *Ma'ariv*, ambayo inafanyika baada tu ya jua kutua. Huduma ya *ma'ariv* inaweza kudumu hadi saa za jioni. Neno *'ereb* linamaanisha *jioni; beny*, kihusishi kilicho kati *ha*, ni *definite article* katika Kiebrania; *'arbayim, jioni, duskiness*. Neno linamaanisha katika jioni- KATI YA KUTUA KWA JUA NA GIZA.

Tatizo la watu fulani wanaofanya masomo ya maneno ni kuchukua maneno hayo nje ya muktadha na kuyatolea ufafanuzi ambao walimaanisha kumaanisha lugha.

Miaka iliyopita, kulikuwa na mtu ambaye alifanya utafsiri wa Agano Jipya, na akaiita **Concordant Version**. Inaonekana, hakujua chochote kuhusu lugha ya Kigiriki. Alichukua **Strong Concordance** na kutafsiri kila neno katika Agano Jipya. Ni fundisho la uongo kama nini lililotokana na mradi huo! Lakini aliichapisha, na hiyo ikamfanya kuonekana kama msomi, kwa sababu tu alichapisha kitabu. Toleo bado linajitokeza mara kwa mara kati ya dini za kupinga utamaduni. Ninapenda kutomiliki nakala. Utafsiri wa Biblia sio mchezo, burudani au hobby. Ni jitihada yenye makini sana, kwa sababu uzima wa milele wa binadamu uko hatarini! Lazima tuthibitishe ukweli na kuushikilia kabisa.

Kisha, ni kipengele kipi cha wakati tunapata kimeunganishwa na neno *beny ha'arbayim*? Kutoka mlango wa 30 inatuambia. Huu ni muktadha katika ambao istilahi hii lazima ieleweke. ***"Na Haruni atafukiza uvumba wa manukato juu yake, kila asubuhi atakapozitengeneza zile taa, ataufukiza. Na Haruni atakapoziwasha zile taa wakati wa jioni*** [*beyn ha'arbayim*] ***ataufukiza, uwe uvumba wa daima mbele za Yahweh katika vizazi vyenu vyote."***[1](Kutoka 30:7-8). Ni lini mtu anawasha taa? Ni wazi, wakati wa machweo.

Nililelewa katika enzi tofauti na wasomaji wengi. Siruhusu taa za umeme ziwake kama wanavyofanya wengi wa kizazi kipya, kwa sababu nilifunzwa kuhifadhi. Hiyo inamaanisha geuza swichi



ya taa ya umeme iwe mahali pa kuzima kila unapotoka kwenye chumba. Nilipokuwa mvulana, hatukuwa na taa za umeme. Tulikuwa na taa za mafuta ya taa. Mamangu angetayarsha taa ya mafuta ya taa kwa kuosha globu ya kioo, kujaza hifadhi ya mafuta taa wakati wa mchana wakati kulikuwa bado na mwanga wa kutosha wa kuona wa jua, na, kisha, katika machweo na hata katika jioni kulingana na kiasi cha mwanga angani, angewasha taa ya mafuta taa. Unajua taa hizo za mafuta ya taa ziliwaka tu kwa masaa kadhaa, na kisha, ilibidi ama uongeze mafuta ya taa zaidi ndani, au uende kwa kitanda. Kwa kawaida tulichukua hiyo njia ya baadaye kwa sababu hakukuwa na pesa nyingi hivyo za kuharibu katika Unyogovu Mkuu nilipokuwa kijana. (Niliona baadhi ya picha za zamani ambazo zilichukuliwa wakati wa Unyogovu. Marafiki, jamaa, na masahibu wangekuja kututembelea na kupiga picha [hatukumiliki kamera], na kisha wangetupea chapa. Ninaweza kukumbuka kuoana picha hizi huku nguo zetu zikiwa na kiraka juu ya kiraka. Hatukuwa na pesa nyingi kununua hata mahitaji. Unyogovu ulikuwa enzi mbaya sana.)

Tunapaswa kuzingatia kwamba katika jioni ni wakati Haruni aliwasha taa, sio baada ya jua kupita kilele chake baada tu ya saa sita. Hilo ndilo *beyn ha'arbayim* linamaanisha, katika jioni wakati taa ziliwashwa. Wakati alichoma uvumba (asubuhi), alitayarisha taa kwa ajili ya kuwashwa jioni, wakati alianza kuchoma uvumba. Ni jambo la kudumu mbele za Yahweh.

Kisha rejeleo lingine la kimaandiko ni Kutoka 29:39. ***Mwana-kondoo mmoja utamchinja asubuhi; na mwana-kondoo wa pili utamchinja jioni...."*** Asubuhi katika Kiebrania ni neno *boqer*, na maana yake ni wakati wa kuchomoza kwa jua. Mwana-kondoo mwingine angetolewa wakati wa kinyume kwa macheo ambayo ni machweo- katika Kiebrania *beny ha 'arbayim*. Tena, neno lile lile linalozingatiwa linatumika hapa.

***Neno la Yahweh liko wazi kabisa na la uwazi sana hivi kwamba akili ya mtoto inaweza kulifahamu!***

Rejeleo lingine ni katika mstari wa 41, ***"Na huyo mwana-kondoo wa pili utamchinja wakati wa jioni*** [*beyn ha'arbayim* jioni]***, nawe utamfanyia vivyo kama ile sadaka ya unga ya asubuhi, na kama ile sadaka yake ya kinywaji, iwe harufu nzuri, ni dhabihu ya kusongezwa kwa Yahweh kwa njia ya moto."***

Kifungu kinazungumza kuhusu dhabihu ya asubuhi na ya jioni. Wakati wa kuchomoza kwa jua na katika machweo sio katika saa tisa alasiri, sio katika saa saba baada ya jua kupita kilele chake, lakini dhabihu ilikusudiwa kuashiria migawanyiko miwili ya siku- siku ya kimaandiko inapoanza machweo, jioni, na wakati sehemu ya mwanga ya siku inaanza asubuhi katika macheo. Rahisi kabisa namna gani! Unaona mafundisho haya safi kwa macho yako mwenyewe kutoka kwa muktadha!

Neno sawa linatumika katika Hesabu 28:8. ***"Na mwana-kondoo wa pili utamsongeza wakati wa jioni*** [*beyn ha'arbayim*]***; kama ile sadaka ya unga iliyosongezwa asubuhi*** [*boqer*]***, na kama sadaka yake ya kinywaji, ndivyo utakavyoisongeza, ni sadaka ya kusongezwa kwa moto, ni harufu ya kupendeza kwa Yahweh."***

Nani sasa anaelewa maana ya neno *jioni* kwa usahihi? Mwandishi amechukua katika uzingatiaji leksimu nyingi za Kiebrania, pamoja na muktadha. Tumechukua muktadha wa kila kifungu na kila kimoja kinatuambia kwamba neno *beyn ha'arbayim* lazima lina maana ya JIONI, BAADA YA JUA KUTUA.

## UTHIBITISHO 4

Pasaka na sikukuu ya Mikate isiyotiwa Chachu ni tofauti. Zinahesabiwa kwa ajili yetu kwa kuangalia sana katika Biblia katika Hesabu 28:16-25. ***"Tena, mwezi wa kwanza, siku ya kumi na nne ya mwezi, ni pasaka ya Yahweh."*** Kusoma kifungu kama kilivyosimama, tunaona Pasaka ya Yahweh inamaanisha siku ambayo Mwangamizi alipita juu ya nyumba za Waisraeli na kumuua mzaliwa wa kwanza wa Kimisri. Siku hiyo ilipata jina lake kutokana na kitendo cha YAHWEH KUPITA juu na kuwaacha Israeli wasihukumiwe, kwa sababu aliona damu kwenye milango ya Waisraeli.

Mstari wa 17 unasoma, ***"Na siku ya kumi na tano ya mwezi huo patakuwa na sikukuu*** [Kiebrania- *chag*]***; mkate usiotiwa chachu utaliwa muda wa siku saba"*** Neno sikukuu limetolewa kutoka kwa neno *chagag*

#2287, mzizi mkuu unaomaanisha *kukusanyika* (kusogea kwenye duara, kuandamana kwa maandamano matakatifu, kuadhimisha sherehe). Kwa hiyo, inawakilisha kusanyiko takatifu. Kusanyiko, *mikra qodesh* kwa Kiebrania, ina maana *wakati watu wanaitwa pamoja kwa ajili ya mkutano mtakatifu*. Mstari wa 18 unasoma, ***"Siku ya kwanza patakuwa na kusanyiko takatifu*** [mikra qodesh- wito mtakatifu pamoja] ***hamtafanya kazi yoyote ya utumishi…."*** Lakini Israeli aliagizwa kutoa matoleo mahususi. Mstari wa 25 unasoma, ***"Na siku ya saba mtakuwa na kusanyiko takatifu; hamtafanya kazi yoyote ya utumishi."*** Siku ya 15 ya Abibu ni takatifu, ya 16 ni sehemu ya Sikukuu, kama zilivyo ya 17, 18, 19, 20. Siku ya 7, siku ya 21 ya mwezi wa Abibu ni siku nyingine takatifu. Ni vipi mtu yeyote ataelewa vibaya? Neno la Yahweh liko wazi kabisa na la uwazi sana hivi kwamba akili ya mtoto inaweza kulifahamu!

## UTHIBITISHO 5

Pasaka na Sikukuu ya Mikate isiyotiwa chachu pamoja hufanya maadhimisho ya siku nane. Fungua Kumbukumbu la Torati sura ya 16, kuanzia mstari wa 1, ambapo tunasoma: ***"Utunze mwezi wa Abibu…."*** Kama nilivyoonyesha mara kwa mara, tafsiri halisi ya kifungu hiki ni, *"Tazama mwandamo wa mwezi wa masuke ya kijani*." Tunatii maagizo haya kila mwaka, tunapotazama kuonekana kwa mwezi mpevu wa majira ya kuchipua.

***"Ukamfanyie pasaka Yahweh, Elohim wako, kwa kuwa ilikuwa ni mwezi wa Abibu alipokutoa Misri usiku Yahweh; Elohim wako. Nawe umchinjie Pasaka Yahweh Elohim wako…."*** Ni lini Yahweh aliwatoa Waisraeli kutoka Misri? Hatuwezi kukosa jambo hilo muhimu. Aliwatoa usiku (mstari wa 1). Israeli walitoka- walifanya kutoka kwao kutoka- Misri usiku na kipengele hicho kwa hakika ni cha maana.***"Huu ndio usiku wa Yahweh, ambao wapasa kuangaliwa sana na wana wa Israeli wote katika vizazi vyao."*** Tunasoma katika Kutoka sura ya 12:42. Kwa nini? **KWA SABABU YA KUWATOA KATIKA NCHI YA MISRI!**

Kuendelea na mstari wa 2 tunasoma, ***"Nawe umchinjie pasaka Yahweh, Elohim wako, katika kundi la kondoo na la ng'ombe mahali atakapochagua Yahweh apakalishe jina lake. Usimle pamoja na mikate iliyotiwa chachu; siku saba utakula naye mikate isiyotiwa chachu…."*** Kiwakilishi kinawakilisha nini? Je, jina la awali la neno "naye (*it*)" ni gani? Ni dhahiri maana iliyokusudiwa ni PASAKA. Msile mkate uliotiwa chachu pamoja na Pasaka.

Pasaka kila wakati hutajwa kama siku ya 14 ya Abibu, kamwe si ya 15, kwa sababu Yahweh alipita juu ya nyumba za Waisraeli. Waisraeli hawangeweza kutekeleza sehemu ya ibada tarehe 14 na kisha kubeba sehemu ya sherehe hadi tarehe 15. Hivyo sivyo Maandiko yanatuambia tufanye.

Kuendelea katika mstari wa 3 tunasoma, "***siku saba utakula naye mikate isiyotiwa chachu***." **HII INA MAANA PAMOJA NA PASAKA.** Kama vile Eusebius alivyosema katika **Ecclesiastical History** (sura ya 23, ukurasa wa 207), kusanyiko la kitume liliweka siku ambayo Wayahudi walitupa chachu (sura ya 24) ili kukumbuka nembo za ukumbusho za kifo cha Messiah, katika Abibu 14. Ni maadhimisho ya siku nane, kama vile kamusi inavyosema. Siku ya 14 ya Abibu ambayo si siku takatifu- lakini Pasaka (inajumuisha mwana-kondoo aliyechomwa na mikate isiyotiwa chachu kwenye meza) ambayo huliwa siku hiyo (Kutoka 12:8). Ya 15, ambayo ni kusanyiko takatifu pamoja na siku za kati, na ya 21 ambayo ni siku takatifu ya mwisho, zinaitwa Sikukuu (*chagag*). Kote katika sikukuu, mkate usiotiwa chachu ni wa kuliwa na chakula chetu.

Kijana mmoja ambaye hakuwa katika mafundisho safi, alitutembelea wakati mmoja hapa Bethel, nanye akasema, "*Vema, sikubaliani na jinsi unavyofundisha Pasaka na Sikukuu*." Nikasema, "*Je, umeisoma kwa akili iliyo wazi? Hebu tuketi na tusome sasa hivi."* Hivyo tukasoma kwa makini kupitia vifungu. Akasema, *"Kumbukumbu la Torati 16 itathibitisha kuwa umekosea."* Nilijibu, "*Vema, tusome kwa makini kupitia Kumbukumbu la Torati 16 nami nitakuonyesha kwamba hujafikiria kwa UMAKINI kifungu hiki."* Niliposoma kupitia mstari wa 3 na kumwonyesha, "***Usimle PAMOJA NA mikate iliyotiwa chachu*** [nomino iliyotangulia ni Pasaka]; ***siku saba*** [ambayo ni sikukuu] **mtakula mkate usiotiwa chachu PAMOJA NAYE** [pamoja na pasaka]***…."*** Akasema, *"Ah, sasa naona unachomaanisha!"* Sijui aliwahi kufanya nini na ujuzi huu, kwa sababu hatujasikia kutoka kwake tangu wakati huo. Hajakuwa katika mawasiliano.

Basi tuendelee na mstari wa 4-6. ***"Wala isionekane kwako chachu muda wa siku saba katika mipaka yako yote; wala katika hiyo nyama uchinjayo siku ya kwanza jioni, kisilale chochote usiku kucha hata asubuhi. Usimle pasaka ndani ya malango yako yote akupayo Yahweh, Elohim wako; ila mahali atakapochagua Yahweh, Elohim wako, apakalishe jina lake, ndipo mtakapomchinja pasaka jioni*** [Kiebrania- beyn

ha'arbayim]***, katika machweo ya jua, kwa wakati kama uliotoka Misri."***1(Kumbukumbu la Torati 16:4-6).

Mahali ambapo Yahweh atachagua inamaanisha kwenda mahali patakatifu ambapo Maskani (au Hekalu baadaye) iko. Hekalu hatimaye lilikuwa katika Yerusalemu. Wayahudi huchukua kuzama kwa jua na kutafsiri kumaanisha wakati jua linapita kilele chake. Wakati wowote baada ya hapo unaweza kuua mwana-kondoo, alasiri ya 14, wanasema. **SI KWELI**!

## UTHIBITISHO 6

Neno la Kiebrania linaloonekana hapa na kutafsiriwa "*kwenda chini*" kwa jua ni *bo'*. Linaonekana kama #935 katika **Strong's Concordance Lexicon**.

Ni neno linalotumika mara nyingi katika Biblia. Linamaanisha *kuingia*. Inathibitishwa na **Holladay's Hebrew Lexicon**, **A Concise Hebrew Aramaic Lexicon of the Old Testament**, iliyochapishwa kwanza mwaka wa 1971 na mara ya pili katika 1974. Neno hilo linamaanisha kuingia au kuja! Wayahudi wana baraka wanazorudia, na wanaziandika kwenye makala mbalimbali ya kidini, kama vile mezzuzas. Utatazama hapo neno la Kiebrania **habayim**. Baraka nzima ya kawaida iliyotafsiriwa kutoka Kiebrania inamaanisha "Heri aingiaye- anayeingia ndani." Tuseme uko hatua moja nje, je umebarikiwa? Bila shaka hapana! Unapaswa kupita mlangoni ili kupokea baraka, lazima uingie ndani.

Neno, kulingana na Holladay, linatumika katika kila mahali pa, *kuingia*, pamoja na kielelezo cha kuishi pamoja. "***Akaingia kwa Hagari...."*** (Mwanzo 16:4). Ibrahimu akaingia kwa Hagari, n.k. Je, hiyo inamaanisha nini? Je, mwanamume anafanya mapenzi na mwanamke hadharani? Watu wanaweza kufanya hivyo leo, lakini hawakufanya hivyo katika nyakati za kale. Neno *bo'* humaanisha *wakati jua linapoingia au kuzama chini ya upeo wa macho na mtu hawezi tena kuliona jua*. Hapa sasa tunaweza kutambua kwa kina zaidi sababu ya matumizi ya usemi wa Kiebrania *beyn ha'arbayim.* Kati ya wakati ambapo jua linazama kwenye upeo wa macho na huwezi kuliona tena (wakati siku mpya ya kimaandiko inaanza) na giza totoro kuingia, ni wakati wa *beyn ha'arbayim*, na neno hilo linamaanisha machweo (kati ya machweo na *giza*). Hilo ndilo usemi unawakilisha: wakati wa machweo, jioni.

**HATUTAACHA KABISA KWA HOJA HII.** Inamaanisha kwamba wakati jua limeingia kwenye upeo wa macho na siku mpya ya kimaandiko imeanza, wana-kondoo wa pasaka walipaswa kutolewa dhabihu. Sabato haianzi baada ya jua kupita kilele. Huko sio "kuingia" kwa jua. Tunaitunza sabato kuanzia machweo hadi machweo ya jua, wakati jua linazama chini ya upeo wa macho, na **HIYO NI SAHIHI NA BARABARA**. Hakuna ubishi kuhusu jinsi ya kutunza Sabato. **HIVYO NDIVYO PIA PASAKA INAPASWA KUHESABIWA**.

Baini mstari wa 8, ***"Siku sita utakula mikate isiyotiwa chachu; na siku ya saba na uwe mkutano mtukufu kwa Yahweh, Elohim wako, usifanye kazi yoyote."*** (Kumbukumbu la Torati 16:8). Wakati mwingine, watu huja na mawazo ya ajabu juu ya maana ya kifungu hiki. Wanasema, "*Siku sita mtakula mikate isiyotiwa chachu, na hiyo inamaanisha kuwa siku ya saba huhitaji kula mkate usiotiwa chachu*." Ikiwa hutakiwi kufanya kazi yoyote, unawezaje kuoka mkate uliotiwa chachu siku ya saba? Bila shaka, baadhi ya washiriki wa Assemblies of Yahweh ni wanahisabati, na wangeweza kusema, "*Hesabu, fizikia na hesabu kwa ujumla zingekuwaje ikiwa ungekuwa mzembe sana kutumia vitabu vya hisabati, calculus, na fizikia?"* Wanafunzi bila shaka wangemaliza kazi kwa sifuri kwa kila mtihani. Kwa hivyo, hatuwezi kubadilisha maana ya kifungu hiki, ili kupingana na vifungu vingine vyote tunavyooanisha navyo. Siku sita kujumlisha moja inamaanisha siku saba za Sikukuu, lakini msisitizo hapa katika siku ya **SABA** wakati kusanyiko takatifu linatunzwa. SNB

***Tunaitunza sabato kuanzia machweo hadi machweo ya jua, wakati jua linazama chini ya upeo wa macho, na HIYO NI SAHIHI NA BARABARA. Hakuna ubishi kuhusu jinsi ya kutunza Sabato.***

Tafuta Ukweli 12 usio na Makosa, sehemu ya 2 katika toleo lijalo la **The Sacred Name Broadcaster**

# ALAMA YA MKATE USIOTIWA CHACHU



**na Mzee Jacob O. Meyer**

[Nakala hii kiasili ilichapishwa katika toleo la Julai-Agosti 1970 la **The Sacred Name Broadcaster**.]

Alama ya Baba yetu wa Mbinguni ambayo anaweka juu ya watu Wake, kama kinyume na alama ya Mnyama- bila shaka itaweza kumaanisha tofauti kati ya wokovu wako wa milele au uharibifu wako wa milele, ndani ya miaka michache, mifupi kutoka sasa. Katika sehemu ya mwisho tulizingatia vifungu kutoka Kumbukumbu la Torati 6 na 11 ambavyo vinaonyesha wazi kwamba alama ambayo Baba yetu wa Mbinguni anaweka katika vipaji vya nyuso zetu na katika mikono yetu ni utiifu kwa sheria Zake, amri Zake, kanuni, na hukumu, kama zilivyorekodiwa katika *Pentateuch* (vitabu vya kwanza vitano vya Agano la Kale). Mara ya kwanza mimi binafsi nilikuja kutambua fundisho hili, nilishtuka tu kwa maana iliyopo katika vifungu hivi.

Kutoka kwa ujana wangu, nimefundishwa kwamba amri za Agano la Kale zote zilibatilishwa kabisa wakati Mwokozi alikufa juu ya mti wa Kalvari. Nilikuwa nimeketi katika huduma nyingi, ambapo watumishi walihubiri kwamba Sheria ya Yahweh ilikuwa nira ya utumwa, kwamba ilikuwa kitu fulani ambacho hakingeweza kamwe kutufanya sisi waadilifu, na kwamba Baba yetu wa mbinguni alikuwa ameianzisha kwa muda kidogo wa wakati.

Baada ya kuanza kutafiti Biblia kwangu mwenyewe, nilikuja kugundua kwamba Mwokozi wetu kamwe hakuaonyesha chochote kama hicho (ama wazi au fiche) kwa wakati wowote, katika huduma Yake. Kwa kweli tunasoma kinyume sana katika Mathayo 5:17-20, ***"Msidhani ya kuwa nilikuja kuitangua torati au manabii: la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amini, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka kutoka kwa sheria, hata yote yatimie. Basi mtu yeyote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha, huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni. Maana nawaambia ya kwamba, Haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni."***

Hili ni karibu hasa kinyume kabisa kwa mafundisho ya kawaida ya madhehebu mengi ya Wakr-sto. Ukr-sto kawaida unasoma mistari ya kwanza ya kifungu hapo juu na kisha wanakuwa wamekengeushwa katika utafsiri wao. Wanafikiria kwamba "kutimiza" inamaanisha "kubatilishwa au kufutwa." Walakini, mabaki ya kifungu hiki yanaonyesha wazi kabisa kwamba utafsiri kama huo hauwezi kabisa kuambatanishwa kwa ushauri wa Mwokozi.

Vipi mtu anaweza KUFANYA na KUFUNZA amri pasipo kuzitii kabisa, kwa uwezo wao

kabisa? Geuka nyuma kwa Isaya 42:21, ***"Yahweh akapendezwa, kwa ajili ya haki yake, kuitukuza sheria, na kuifanya iheshimike."*** Hili ni Neno la Yahweh! Maagizo haya yanaonyesha kwako, kwamba Mwenye-nguvu Yahweh, Baba wa Mbinguni, angewahi kufikiria kubatilisha amri ambazo alikuwa ametoa?

Pia tunasoma katika kifungu kinachojulikana kawaida kama Amri 10, kinachopatikana katika Kutoka 20:5-6, ***"...Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, Yahweh Elohim wako, ni El mwenye wivu, nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu."***

Nikiwa mvulana shuleni, nilijifuza Amri 10 kama mazoezi katika ushairi. Kama inavyofanyika mara nyingi, nilisoma katika maagizo haya bila hata kugundua yalimaanisha kwamba mimi, mimi mwenyewe nilipaswa kuwa natii maneno haya ya Mwenye-nguvu Yahweh! Inaonekana kwamba wakati fulani tunasoma mambo mengi muhimu katika Biblia pasipo kuelewa kabisa nini tunayosoma!

Hivyo basi tunafikia kwa maandishi ya Mtume Paulo. Bila ubaguzi, na ninarudia, BILA UBAGUZI, maandishi ya Paulo yanatumiwa na wanatheolojia wa Ukr-sto kuthibitisha kukataa kwao kwa amri za Yahweh! Unaamini hata kwa dakika moja kwamba Paulo angeweza kusema kitu fulani ambacho kilikuwa kinyume kabisa kwa yale kichwa cha mwili, Yahshua aliye Messiah, alikuwa akifundisha? Unaweza kufikiria kwamba wanaume ambao walikuwa wameteuliwa kuhuburi Neno, wangekuja mbele kwa ujasiri na kusema kwamba Mtume Paulo alianzisha dini mpya? Lakini hili ndilo hasa lililopo katika vitabu vya theoloji, nilivyo navyo katika maktaba yangu. Paulo alikuwa nani, hata hivyo? Hakuwa rabi katika Uyahudi, kwani alisoma chini ya Rabi maarufu Gamalieli? Angalia Matendo ya Mitume 22:3, 23:6, na Wafilipi 3:5.

Unajua kwamba yoyote ya vifungu ambavyo kwa kawaida vinanukuliwa kutoka kwa maandishi ya Mtume Paulo kuthibitisha mafundisho ya hakuna-sheria, kwa kweli vinafundisha utunzaji wa sheria vinapochukuliwa katika muktadha. Bila ubaguzi, kama utapata mtu fulani akifundisha mafundisho ya hakuna-sheria, mtu huyo anasoma mstari mmoja au kirai ambacho hakimaanishi katika muktadha yale yanayowasilishwa kumaanisha. Kwa mfano Waefeso 2:8-9, kila mara inawekwa nje wakati majadiliano ya amri za Yahweh na umuhimu Wake kuhusiana kwa Ukr-sto wa kisasa yanatokea. Inasoma, ***"Kwa maana mmeokolewa kwa neema kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Yahweh; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."*** Na kisha wanasimama baada ya mstari huu na kufafanua kwa nguvu juu ya hatari za kutii Sheria za Yahweh, pengine wakisema kwamba hakuna yoyote atakayeokolewa ikiwa anatii amri za Yahweh. Wanajaribu kuthibitisha kwamba kushika amri kamwe haitasimama katika njia yao- wanatoka nje ya njia yao kuishi kinyume na amri.

Lakini subiri! Mstari unaofuata unaelezea: ***"Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Messiah Yahshua, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Yahweh aliyatengeneza ili tuenende nayo."*** Sasa tunalo neno- "kazi" na "kazi". Moja ya seti hizi za "kazi" hakika ilibatilishwa wakati Mwokozi alikufa. Seti nyingine ya "kazi" iliteuliwa kabla ya seti ya pili ya "kazi" na tunapaswa kutembea na kuishi katika kazi hizi. Ni rahisi kuelewa kama hatutajaribu kuweka utafsiri wetu wenyewe. Msimbo mmoja wa sheria ulikuwepo kutoka Adamu na ulitiiwa na wazee wote. Msimbo mwingine wa Sheria- kumaanisha Sheria za dhabihu- zilibadilishwa wakati Mwokozi alikufa.

Ningetaka kwamba watu hao wote ambao wanafunza mafundisho ya hakuna-sheria wangeenda kwanza kwa Warumi 3:31 kabla ya kuamua kwamba amri za Yahweh zilibatilishwa wakati Mwokozi alikufa, au zilibadilishwa baadae na Paulo. Huyu anayedhaniwa kuwa mhubiri wa hakuna-sheria anasema tu katika kifungu hiki, ***"Basi, je, twaibatilisha sheria kwa Imani hiyo? Hasha! twaithibitisha sheria."*** Pia tunapata mifano mingi katika kitabu cha Matendo ya Mitume ambapo Paulo kwa kweli anatambua kwamba alikuwa akihubiri utiifu badala ya uasi dhidi ya Sheria ya Yahweh.

Usijaribu kusisitiza kwamba amri za Yahweh zilikuwa za Wayahudi pekee, kwa sababu sehemu ya mwisho ya Waefeso mlango wa 2 inasema kwamba kiambaza cha kati kilichotutenga kilivunjwa kati ya Mataifa na Wayahudi na wote wamefanywa mmoja kwa kifo cha Messiah, juu ya mti wa Kalvari. Tambua pia Isaya 56:1-8.

Katika muktadha huu ningependa kuleta alama moja tu kwa tahadhari yako ambayo Baba yetu wa Mbinguni ameweka juu ya watu Wake. Tunasoma kuhusu alama hii katika Kutoka mlango wa 13. Kifungu hiki kinashughulika na Sikukuu ya Mikate isiyotiwa Chachu. Tunaambiwa katika kifungu hiki kwamba kwa siku saba kila mwaka tunahitajika kutupa chachu yote nje ya nyumba zetu na tule mkate usiotiwa chachu pekee pamoja na

chakula chetu.

Tunasoma katika mistari ya 7 hadi 10, ***"Mikate isiyochachwa italiwa katika hizo siku saba; mkate uliotiwa chachu usionekane kwako, wala chachu isionekane kwako, ndani ya mipaka yako yote. Nawe utamwambia mwanao siku hiyo, ukisema, ni kwa sababu ya hayo Yahweh aliyonifanyia hapo nilipotoka Misri. Nayo itakuwa ishara kwako katika mkono wako, na kwa ukumbusho kati ya macho yako, ili kwamba sheria ya Yahweh ipate kuwa kinywani mwako; kwani Yahweh alikutoa utoke Misri kwa mkono wenye uwezo. Kwa hiyo utaitunza amri hii kwa wakati wake mwaka baada ya mwaka."***

Umeona kwamba kwa kuadhimisha Sikukuu ya Mkate Usiotiwa Chachu, inajumuisha ishara ambayo Mwenye-nguvu Yahweh anaweka juu ya watu Wake? Kwa kuchukua chachu kutoka kwa nyumba zetu kwa siku saba, ishara ya Yahweh inawekwa juu ya mkono wetu, ambayo inaashiria jinsi tunapata riziki yetu, au vinginevyo kutumia ustadi wetu, na kwa kumbukumbu katikati ya macho yetu, ambayo inahusiana kwa kiti cha akili inayotawala mwenendo wetu wote. Tena katika mstari wa 16 tunapata marejeleo kwa alama hii. Tunasoma hapa, ***"Jambo hilo litakuwa ni ISHARA MKONONI MWAKO, na UTEPE KATIKATI YA MACHO YAKO; KWA KUWA YAHWEH ALITUTOA MISRI KWA UWEZO WA MKONO WAKE."***

Nini tu utafsiri wa kimaandiko wa chachu? Katika maandishi ya Kiebrania maneno yafuatayo yanatumiwa: *se'or* na *chamets*. Yanamaanisha *chachu au unga wa siki*, ambayo inafura na kuchachuka. Chachu huharibika au kuoza. Kwa sababu hiyo, tunajifunza kwamba chachu inawakilisha ushawishi wa uharibifu katika maisha yetu, ambayo pia inatufanya wachafu kimaadili, na inakua mara kwa mara isipokuwa imeng'olewa. Chachu inawakilisha mafundisho ya uongo, ambayo yanaelekeza kwa dhambi.

Katika Mathayo 16:6 tunapata kwamba Yahshua aliye Messiah anawahimiza wanafunzi Wake kujihadhari kwa chachu ya Mafarisayo na Masadukayo. Katika mstari wa 12 walielewa onyo lake kumaanisha kwamba wanapaswa kujihadhari kwa MAFUNDISHO (kufundisha) ya Mafarisayo na Masadukayo. Pia tunapata tukio katika Mariko 8:15 ambapo Yahshua aliye Messiah, Mwokozi wetu, anatuonya dhidi ya chachu ya Herode, kumaanisha muungano wa karibu kati ya nyanja za kisiasi na serikali za kidini.

Chachu inawakilisha mafundisho ya uongo, ambayo kama yatafuatwa, yanatuongoza sisi kuishi maisha yetu kinyume kwa Mapenzi na matakwa ya mwenye-nguvu Yahweh. Kama tutafuata mafundisho ya uongo, tutakuwa wenye hatia kwa dhambi.Mafundisho ya uongo yanaongoza kwa dhambi kwa sababu yanatuongoza sisi kwenye njia ambazo ni kinyume kwa njia ambayo Mwenye-nguvu Yahweh ametuelekeza kwamba tutembelee ndani yake.

Wakati Mwenye-nguvu Yahweh, katika Neno Lake anatuambia tusafishe nyumba zetu kwa chachu zote- kuweka chachu zote nje ya nyumba zetu- anamaanisha kwamba lazima tuwe WASOMAJI WA LEBO kwa wiki. Tutaweka imani yetu chini ya uchunguzi wa karibu, kama tunalinganisha imani yetu na Maandiko yaliyoongozwa. Kama tunakagua na kuchunguza vyakula vyote tunavyochukua ndani ya manyumba yetu, wakati huo sawa, tunakuwa na ufahamu kwa chochote ambacho ndani yake tunaweza kupotoka, kwa njia ndogo zaidi, kutoka kwa amri ambazo Mwenye-nguvu Yahweh, katika Neno Lake, alituamuru tutunze.

Kama yu mmoja wa watu hawa ambao wanayo maoni kwamba Sikukuu ya Mkate Usiotiwa Chachu ilibatilishwa wakati Mwokozi alikufa juu ya mti wa Kalvari, ruhusu mimi nielekeze makini yako kwa 1 Wakorintho 5:6-8. Tafadhali baini kwamba haya ni moja ya Maandishi ya Mtume Paulo. Tunasoma hapo, ***"Kujisifu kwenu si kuzuri. Hamjui kwamba chachu kidogo hulichachusha donge zima? Basi, jisafisheni, mkatoe ile chachu ya kale, mpate kuwa donge jipya, kama vile mlivyo hamkutiwa chachu. Kwa maana Pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka, yaani, Messiah; basi na tuifanye sikukuu, si kwa chachu ya kale, wala kwa chachu ya uovu na ubaya, bali kwa yasiyochachika, ndio weupe wa moyo na kweli."*** Wazi kwa ukamilifu namna gani ni kifungu hiki! Hata MTUME PAULO ALITUHIMIZA SISI KUTUNZA ***Sikukuu ya Mkate Usiotiwa Chachu***. Kama ***tunasafisha*** (Kigiriki- *cartharsis*), chachu ya kale ya uovu (maana yake *mabaya*, *ubaya*, *uzinzi* au *upotovu*), *uovu* (maana yake *upotovu*, *dhambi* au *uovu*,) na uvunjaji wa Sheria, kama utapenda.

Kama tutafanya haya, basi tutakuwa watu wa Yahweh na ataandika alama Yake juu ya mkono wetu na katika paji la uso, kuonyesha kwamba ni Yeye Mwenye-nguvu Yahweh, Mwenyewe, ambaye anatuongoza sisi na maishi yetu.

Vipi kuhusu wewe? Wewe ni mmoja wa watu wa Yahweh? Maisha yake yanaweza kubadilika na unaweza kuwa mmoja wa watoto Wake leo, kama utaanza sasa kumtii Yeye. SNB



# Mapishi ya Siku za Mikate Isiyotiwa Chachu

## Passover Bread

Ingredients:

- Maziwa Pints 3
- Pouni moja ya siagi
- Unga

Kwa kutumia processor ya chakula, changanya maziwa na siagi, kisha ongeza unga mwingi kadri inavyohitajika ili kuupa mwili sawa na unga wa pai. Gawanya katika sehemu nne na ufanyie kazi kila moja hadi iwe malengelenge; kisha songa kwa unene wa unga wa pai. Kata vipande 2'X4'. Piga alama au choma kwa uma (kama ganda la pai). Oka kwa 350°F hadi iwe rangi ya hudhurungi kwenye kingo.

Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu ni wakati wa pekee sana wa mwaka. Wakati wa siku takatifu, mlo wetu lazima ubadilishwe ili kutimiza mahitaji yote ya kimaandiko ya sikukuu hii. Ni lazima tuondoe chachu zote (Kiebrania- Se'or na chametz, ikimaanisha chachu, barm, kuvimba au kuharibika) kutoka kwa maisha yetu ya kila siku. Hii inajumuisha vyanzo vyote vya chakula na bidhaa zote tunazotumia majumbani mwetu na kwenye miili yetu kama vile deodorants, dawa ya meno, vitamini, sabuni, bia, soda, hata chakula cha mbwa n.k. Haya ni makaazi yetu na hakuna bidhaa yoyote ya chachu inayoweza kuonekana katika sehemu zetu zote (kutoka 12:15-19). Pombe ya nafaka (wakati mwingine hutumiwa katika bidhaa kama vile vanila) na siki iliyotiwa maguta pia ni marufuku.

Dawa hizi za chachu huonekana chini ya majina kama vile chachu (ya waokaji na watengenezaji wa pombe), poda ya kuoka, soda ya kuoka (bicarbonate ya Sodiamu), chachu, barm (chachu), cream ya tartar, au majina mengine.

Viungo hivi vinaweza kutokea katika vitu kama vile unga wa sabuni unaotumwa wa sabuni, supu (ya makopo, kavu, au bouillon), keki ya chakula cha malaika, chumvi ya meza, vitamin, mkate, crackers, biskuti, keki, soda pop, bia, na kadhalika. Orodha hii ni kubwa, lakini ni muhimu kwamba sisi kama Waabudu wa Kweli tutoe chachu YOTE nje (Kutoka 12:15, 19 na Kumbukumbu la torati 16:4). Usisahau makombo katika toaster au mfuko wa kusafisha wa vacuum (baada ya kusafisha yote). Hakikisha umesoma kila lebo kwenye vyombo vyote vya bidhaa nyumbani kwako. Vitu hivi vyote vinapaswa kuondolewa kutoka kwa nyumba yako (mali). Tazama Kutoka 13:7 na 1 Wakorintho 5:8-huwezi kuzihifadhi kwa matumizi ya baadaye. Kumbuka kuanza mapema, ukiangalia viungo vyote kwenye kila ununuzi unaofanya, na kila kitu nyumbani mwako. (Kwa nini usiwe msomaji wa lebo kwa mwaka mzima ili uweze kutii Sheria za lishe za Yahweh?)

Ili kufanya Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu kuwa wakati maalum, mapishi yafuatayo yamejumuishwa katika chapisho hili. Furahia Kula! SNB

***Mapishi haya mengi na mengine yanaweza kupatikana katika Assemblies of Yahweh Cookbook. Kwa maelezo ya bei, tafadhali andika kwa: Assemblies of Yahweh, PO Box C, Bethel, PA 19507***




## Whole Wheat Oatmeal Crackers

Vijiko 2 vya asali
kikombe cha mafuta
kikombe cha maziwa
vikombe 2 vya unga wa ngano
Vikombe 1½ vya oatmeal
¼ vijiko 2 vya unga wa soy
2/3 kijiko ½ cha chumvi

Changanya asali, mafuta na vinywaji. Koroga viungo, changanya vizuri. Kanda kwa dakika 5. Pindua kwenye karatasi ya nta hadi 1/4", peleka kwenye karatasi ya kuki iliyotiwa mafuta. Kata kwa maumbo au vipande unavyotaka, kisha uchome kwa uma. Oka kwa 350° kwa dakika 12-15 au hadi rangi ya dhahabu.

## Creamy Italian White Bean Soup

Wakia 14 za maharagwe ya cannellini
Sehemu 5 za vitunguu saumu zilizokatwa
Vikombe 2 vya mchuzi wa kuku au mboga
Kopo 1 ya mchicha uliokaushwa au vikombe 4 vya mchicha safi
Vipande vya pilipili nyekundu

Chota vijiko 2 vya maharagwe kutoka kwenye kopo na kuweka kando. Ponda maharagwe yaliyobaki. Katika sufuria ya wastani, kaanga vitunguu saumu hadi kiwe na rangi ya uwazi, kisha ongeza mchuzi na mchicha. Chemsha kwa dakika 15. Ongeza maharagwe yaliyopondwa na vipande vya pilipili nyekundu, pika kwa dakika, zaidi. Weka chumvi na pilipili kwa ladha.

## Passover Potato Filling

Mchuzi wa kuku lita 1,
Sanduku 1 ya matzos
Kijiko 1 cha parsley
½ kijiko cha chumvi
Mayai 3
Kijiko cha-chai 1 cha sage
lita 1 moja ya maji
vikombe 3 vya maziwa
fimbo moja ya siagi
kitunguu 1 kikumbwa, kilichokatwa
vipande vya viazi

Chemsha mchuzi, vunjavunja matzos na uongeze kwenye mchuzi. Ongeza kiungo kilichobaki kwenye mchuzi, isipokuwa kwa vipande vya viazi. Ongeza sehemu za viazi mpaka upate unene unaotaka. Oka kwa 350° kwa dakika 45 zimefunikwa na dakika 15 bila kufunikwa.

## Spicy Sephardic Pancakes

Viazi 3,vilivyomenywa
Kitunguu 1 kilichokatwa,
Vijiko 3 vya mafuta ya zeituni
Pauni 1 ya mchicha safi
Mayai 3, yaliyopigwa

½ kijiko cha turmeric
½ kijiko cha chai, cha cumin
1 ½ vijiko vya vitunguu saumu ilikatwakatwa
Chumvi na pilipili ili kuonja
mafuta kwa kukaanga

Chemsha viazi hadi laini, chuja na uponde. Kaanga vitunguu katika mafuta ya zeituni hadi laini. Ondoa shina kutoka kwa mchicha, kisha ukate laini. Ongeza kwa vitunguu, pika kwa dakika 1-2. Weka mchanganyiko kwenye bakuli kubwa, changanya viungo vilivyobaki isipokuwa mafuta ya kukaanga. Pasha mafuta kwenye sufuria kubwa. Kisha ongeza mchanganyiko kwa vijiko ili kuunda pankeki 3''. Kaanga pande zote mbili hadi iwe kahawia. Pakua ikiwa moto.

## Sand Tarts

Vikombe 4 ½ vya unga
Vikombe 2 ½ vya sukari
Pauni 1 ya siagi
Mayai 3

Lainisha siagi kwa joto la kawaida. Changanya siagi na sukari hadi creamy. Ongeza mayai, kisha ongeza unga. Mimina vijiko vikubwa kwenye karatasi ya kuki. Pika dakika 12-15 kwa 400°. Waweza weka juu karanga zilizokatwa vizuri au ziviringishe kwenye mchanganyiko wa sukari ya mdalasini zikiwa moto.

## Artichoke Dip

Kopo la 14 oz. la moyo wa artichoke mioyo
Kopo la 15.5 oz. la maharagwe ya Great North isiyo na kokwa
Vijiko 2 vya mafuta ya mizeituni
thyme kavu
Vijiko 3 vya maji ya limao

2 karafuu vitunguu
mizeituni 6 ya kalamata
kijiko 1 cha-chai cha
chumvi na pilipili ili kuonja

Weka viungo vyote isipokuwa mizeituni kwenye processor ya chakula, ponda mpaka vipande vidogo sana vya artichoke vinaonekana. Ongeza chumvi na pilipili kwa ladha. Weka kwenye bakuli, nyunyizia mafuta juu na upambe na mizeituni ya kalamata. Kutumikia na mkate usiotiwa chachu au mboga za kuchovya.

## Refried Beans

Maharagwe ya pinto ya makopo lita 1
½ kitunguu vya wastani vilivyokatwa
Sehemu 3 ya vitunguu saumu iliyokatwa
Vijiko-vya-chai 1 ½ vya unga wa pilipili
kijiko-cha-chai 1 cha cumin
chumvi na pilipil kwa ladha

Katika sufuria kubwa, weka kijiko cha mafuta ya mizeituni na kaanga vitunguu kwa dakika 3. Ongeza vitunguu na viungo, endelea kukaanga kwa dakika 1. Chuja maharagwe, ukihifadhi kikombe 1 cha kioevu. Ongeza maharagwe na ufanye kichemke na upike kwa dakika 5, ukiongeza kioevu kilichohifadhiwa kama inahitajika. Saga na masher ya viazi au blender ya kuzamisha. Kitamu kilichopakuliwa kwenye tortilla za nafaka za kukaanga au mkate usiotiwa chachu.

## Salmon Cakes

Kopo la 1 1/2 oz. ya samoni wa rangi ya waridi
1/2 kikombe cha vitunguu vilivyokatwa
Yai 1, iliyopigwa kidogo
½ kikombe cha unga

Chuja samoni, changanya na viungo vingine kwenye bakuli ndogo. Gawanya katika patties sita. Kaanga katika mafuta ya moto hadi hudhurungi ya dhahabu. Unaweza kuvingirisha kila keki kwenye mlo wa matzo au mlo wa mahindi kabla ya kukaanga kwa mgandamizo zaidi.

## Matzo Spinach Meat Pie

4 matzo
Pauni 1 ya mchicha, iliyokatwa
Kitunguu 1 cha wastani kilichokatwa
Vijiko 6 vya mafuta
Pauni 1 ya nyama ya kusaga
kijiko1 cha chumvi
bana iliyokatwa ya pilipili ya Jamaika
kikombe 1 cha viazi zilizosokotwa
3 mayai

Loweka matzo ambayo haijavunjika kwenye maji baridi hadi laini, kama dakika mbili. Chuja vizuri kwenye kitambaa cha karatasi. Kaanga vitunguu katika mafuta, kisha ongeza nyama ya kukaanga. Kupika hadi kahawia, kisha kumwaga mafuta ya ziada. Ongeza na chumvi na pilipili ya Jamaika. Changanya mchicha na viazi kwenye mchanganyiko wa nyama. Piga mayai 2 vizuri, kisha mimina juu ya mchanganyiko na mchanganyiko vizuri. Paka sufuria ya mraba mafuta, kisha funika chini ya sufuria na matzos. Eneza mchanganyiko wa nyama juu, kisha funika na matzos mbili. Paka mafuta vijiko 2. Piga yai iliyobaki, ueneze juu ya yote. Oka kwa 400° kwa dakika 50. Hufanya resheni 4-6.

# Homemade Taco Seasoning

Vijiko vinne kila moja:
Unga wa pilipili
Bizari nyembemba
poda ya vitunguu
kijiko ½ cha pilipili nyekundu iliyopondwa

Changanya viungo vyote pamoja na uhifadhi kwenye chombo kisichopitisha hewa. Tumia kwa kuongeza radha nyama ya ng'ombe au bata, au kuku iliyokatwa. Unaweza kuhitaji kuongeza chumvi kwenye mchanganyiko hapo juu kabla ya kuhifadhi.

# Cream of "Something" Soup Mix

Kikombe 1 cha maziwa kavu,
¾ kikombe cha cornstarch
¼ kikombe cha bouillon
Vijiko 4 vya vitunguu vilivyokatwa
kijiko cha basil, thyme, pilipili

Changanya viungo vyote. Ukiwa tayari kutengeneza supu, tumia 1/3 kikombe cha mchanganyiko kavu na vikombe 1 ¼ vya maji. Pika hadi iwe nzito. (Hakikisha umeangalia viambato vya bouillon. Aina nyingi hutumia chachu kama kiungo.) Unaweza kuongeza vionjo kama vile sauteed celery au vitunguu, brokoli iliyokaushwa au asparagus ili kuongeza ladha.

# Lemon Pudding Cake

½ kikombe cha sukari.
vijiko 3 vya unga,
Kijiko 1 cha lemon zest
maji ya limau
Vijiko 2 vya siagi iliyoyeyuka
Viini 2 vya yai vilivyopigwa kidogo,
kikombe 1 cha maziwa,
Ute wa yai 2
whipped cream (ya hiari)

Katika bakuli kubwa la kuchanganya, changanya unga na sukari, kisha ongeza zest ya limao, maji ya limao, na siagi iliyoyeyuka. Koroga viini vya yai na maziwa, ongeza kwenye mchanganyiko. Koroga tu hadi ichanganywe. Katika bakuli tofauti, piga ute wa mayai mpaka kilele kingumu kitengeneze. Kunja ute wa mayai kwa upole kwenye unga wa limao. Weka kwa kijiko kwenye sufuria ya kukata mafuta. Weka sahani kwenye sufuria ya kuoka 13X9. Mimina maji ya moto au maji ya bimba moto zaidi kwenye sufuria karibu na bakuli la bakuli kwa kina cha inchi 1. Oka katika tanuri 350° kwa dakika 40-45. Kutumikia kikiwa moto na whipped cream.

*Sacred Name Broadcaster*
*Bethel, PA 19507*

**PERIODICAL**

Reading, PA

# Vyombo vyako Bora vya Kujifunza Biblia




# WMLK Radio

## Assemblies of Yahweh Shortwave

**Now Broadcasting 6 DAYS A WEEK**

**15150 kHz 1200-1700 GMT (8 AM - 1 PM EDT)**

**17525 kHz 1730-2230 GMT (1:30 PM - 6:30 PM EDT)**

**9275 kHz 2300-0400 GMT (7 PM - 12 Midnight EDT)**

**On the air 24/7 at WMLKRadio.com, on TuneIn.com or at station.voscast.com/5cfe89883c143**

(Note: There are times that WMLK is not broadcasting because of maintenance or repairs.)